JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**SHAURI NA. 25 - 2019/2020**

**DHIDI YA**

**EAST AFRICA RADIO**

**UAMUZI**

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA ZA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA UTANGAZAJI WA REDIO NA TELEVISHENI), 2018.**

## 1.0 MAELEZO KUHUSU UKIUKAJI WA KANUNI

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilitoa leseni ya kurusha Matangazo (Matangazo ya Redio) kwa Kituo cha **EAST AFRICA RADIO** kwa ajili ya kutoa huduma ya utangazaji wa maudhui kwa njia ya Redio.

1.2 Tarehe 28 Mei, 2020 kati ya Saa 12.00 na Saa 3.00 asubuhi**, EAST AFRICA RADIO** kupitia kipindi cha ***Supa Breakfast*** wanatuhumiwa kukiuka Sheria, Kanuni na Maadili ya Utangazaji kwa kurusha maudhui yenye kukashifu utendaji wa Serikali katika uteuzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

1.3 Watangazaji wa kipindi cha ***Supa Breakfast*** walitumia lugha ya kashfa dhidi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa kusema kwamba hana meno katika utendaji wake wa kazi. Watangazaji walisikika wakitoa maelezo hayo kwa lugha ya kukejeli utendaji wa Serikali.

1.4 Maudhui ya kipindi yalikuwa na maoni binafsi ya watangazaji jinsi wanavyoona utendaji wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kushindwa kutoa nafasi kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kutoa maelezo yao dhidi ya tuhuma hizo

kama ni kweli hawana meno katika utekelezaji wa majukumu yao. Watangazaji wa kipindi walisikika wakisema maneno yafuatayo:

***"...jana tulikua tunajadili na Sam kuwa huenda CAG hana meno.... hana meno ndio yale yale...anakagua vitu...kama kila mtu anaweza kumtia vidole tu...anamsokola eh...anampiga masingi...bwana CAG wabunge wamekuombea uwepo wa sheria kali ambayo ikiwezekana sheria iwe na kitengo fulani hivi maalumu ya kuondoka na maaskari na nini..."***

## 2.0 KANUNI ZILIZOKIUKWA

Kwa kitendo cha kutangaza kipindi cha ***Supa Breakfast*** kikiwa na maudhui yenye lugha ya kukashifu pamoja na maoni binafsi ya watangazaji bila ya kutoa nafasi kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa maoni yao, **EAST AFRICA RADIO** inatuhumiwa kukiuka Kanuni Na. 17 (1), 24 (a), (b), (c), na 29 (b) za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018, ambazo zinasomeka kama ifuatavyo:

*17.-(1) Where the licensee allows the expression of personal views during the programme, the audience shall be informed in advance and be given an opportunity to respond to such views.*

*24. A content services licensee providing free-to-air shall ensure that when broadcasting controversial issues of public interest during live broadcasts-*
*(a) a wide range of views and opinions are presented;*
*(b) a person or organization whose views on any controversial issues of public interest has been criticized during the broadcast, and who replies to such criticism within a reasonable time, shall be offered an opportunity by the licensee to reply to such criticism;*
*(c) a reply to criticism under paragraph (b) is given a similar degree of prominence and shall be broadcast on a similar time- slot, as soon as is reasonably possible.*

*29. A content services licensee shall-*
*(b) refrain from using language meant to mislead or unnecessarily cause alarm and despondency;*
*(d) avoid use of indecent and abusive language in programme presentation;*

## 3.0 WITO WA KUTOA MAELEZO YA UTETEZI.

Tarehe 19 Juni, 2020, Kamati ya Maudhui iliuandikia uongozi wa **EAST AFRICA RADIO,** wito wa kuwasilisha utetezi wao wa maandishi pamoja na kufika mbele ya Kamati ya Maudhui kujieleza dhidi ya tuhuma zinazowakabili.

Tarehe 24 Juni, 2020, Uongozi wa **EAST AFRICA RADIO** uliwasilisha utetezi wa maandishi uliosainiwa na **Regina Mengi**, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo. Pia, tarehe hiyo hiyo, Uongozi huo ukiwakilishwa na **Sophia Mnganya**, Mratibu wa TV, **Xavier Maleko**, Wakili wa Kituo pamoja na **Lydia Igarabuza**, Mtayarishaji Vipindi wa Kituo ulifika mbele ya Kamati kutoa utetezi.

## 4.0 UTETEZI WA EAST AFRICA RADIO

Katika utetezi wao wa maandishi, **EAST AFRICA RADIO** walisema kuwa maudhui ya kipindi chao yalihusiana na hoja iliyotolewa Bungeni na Mh. Eng. Christopher Chiza (Mbunge) na dhumuni lao lilikuwa ni kuripoti hoja za Wabunge za kuonesha kwamba kuna uhitaji wa CAG kuongezewa nguvu zaidi kisheria. Walidai kuwa hawakuichukulia hoja ya Mh. Mbunge huyo kama tuhuma ambapo ingewapasa kutafuta maoni ya upande wa pili, yaani Ofisi ya CAG na kuitaka kutoa maelezo yake ingekuwa sawa na kuifanya ijibizane na Bunge. Waliendelea kudai kuwa walitafuta maoni ya mtaalamu, Dkt. Albanie Marcossy kutoka Taasisi ya Kufuatilia Mwenendo wa Bunge.

Walisema kuwa maudhui yao hayakuwa na nia ya kumkashifu CAG bali kuelezea hoja za Mbunge.

Pia, walikiri kwamba watangazaji wao katika sehemu ndogo ya maongezi yao walitumia lugha yenye ukakasi kidogo na kuwa wameshawachukulia watangazaji hao hatua. Walimaliza kwa kuomba radhi na kusema kuwa wanataraji Kamati ya Maudhui haitachukua hatua zaidi dhidi yao ikizingatiwa kuwa ni mara ya kwanza kwa Redio yao kuitwa mbele ya Kamati.

Pia, **EAST AFRICA RADIO** ilitoa utetezi wao wa mdomo kama ifuatavyo

4.1 **Sophia Mnganya** alieleza kwamba wameshachukua hatua za kuwapa onyo na kuwasimamisha kutangaza kipindi husika watangazaji waliotumia lugha ya ukakasi. Alipokuwa akijibu maswali ya Kamati, alisema kuwa nyaraka hizo za onyo hawakufika nazo kwenye Kamati. Pia, alijibu kuwa japokuwa hawajazingatia mizania, bado wanaona kuwa wana muda wa kutafuta maoni ya Ofisi ya CAG na kwamba wapo kwenye mchakato huo. Alimaliza kusema kuwa waligundua kosa kabla ya kupokea wito wa Kamati na kwamba majadiliano yaliyofanyika kwenye Kamati yamewajenga zaidi.

4.2 **Lydia Igarabuza** alisema kuwa katika kipindi hicho kulikuwa na utaratibu wa ndani katika Ofisi yao ambapo walitakiwa kutowaalika wageni studio. Alisema anaomba msamaha kwa Kituo chao kuteleza na kutumia lugha ya mtaani katika kipindi.

4.3 **Xavier Maleko** alisema wanatambua kuwa wamekiuka Kanuni ya 29 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Redio na Televisheni), 2018 ambayo inakataza kutangaza maudhui yasiyo na lugha ya staha. Alimaliza kwa kusema kuwa wanaomba kupewa adhabu ya onyo

tu kwa sababu wameshajifunza kwenye kikao cha Kamati na watajitahidi kutotenda makosa tena.

**5.0 TATHMINI YA KAMATI**

Kutokana na utetezi wa **EAST AFRICA RADIO,** Kamati imetoa tathmini ifuatayo: -

5.1 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba **EAST AFRICA RADIO** imefanya kosa la kutangaza maudhui yenye lugha ya kukashifu pamoja na maoni binafsi ya watangazaji bila ya kutoa nafasi kwa Ofisi ya CAG kutoa maoni/maelezo yao, kama ambavyo wamekiri wenyewe, kinyume na Kanuni Na. 17 (1), 24 (a), (b), (c), na 29 (b) za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018;

5.2 Kamati ya Maudhui imeona kuwa madai ya **EAST AFRICA RADIO** kuwa maudhui yao yalihusu hoja iliyojadiliwa na Wabunge haina mashiko kwa sababu ni wazi kuwa Wabunge hawakuongelea hoja hiyo kwa lugha ya kashfa wala tuhuma bali wao **EAST AFRICA RADIO** ndiyo walifanya hivyo. Katika mazingira hayo, **EAST AFRICA RADIO** walitakiwa kuipa nafasi ofisi ya CAG ili kutoa maoni/maelezo yao katika kipindi kile kile walichotolea tuhuma dhidi yao. Habari yao ilipaswa kuwa na mizania;

5.3 Pia, Kamati ya Maudhui imebaini kuwa utetezi wa **EAST AFRICA RADIO** kuwa bado wana muda wa kuialika ofisi ya CAG kutoa ufafanuzi si ya msingi kwa sababu Sheria inawataka kuzingatia mizania kwa kuipa nafasi Ofisi ya CAG kutoa ufafanuzi wao katika kipindi kile kile walichotumia kutolea tuhuma. Umepita mwezi mmoja sasa tangu watangaze tuhuma hizo bila ya kuipa nafasi Ofisi ya CAG;

5.4 Kamati haikubaliani na utetezi wa **EAST AFRICA RADIO** kuwa walimualika Dkt. Albanie Marcossy kutoa ufafanuzi wa tuhuma walizotangaza kwa sababu Sheria inawataka waialike Ofisi husika iliyoelekezewa tuhuma kutoa maoni/ maelezo yao.

**6.0 USHAURI WA KAMATI KWA EAST AFRICA RADIO.**

Kutokana na makosa yaliyobainika, Kamati inaushauri Uongozi wa **EAST AFRICA RADIO** kuhakikisha wanawapatia watangazaji wao mafunzo ya mara kwa mara ya Utangazaji wa Habari ili kuweza kuepuka kutenda makosa yanayoweza kuzuilika na kuimarisha utendaji wao.

**7.0 UAMUZI WA KAMATI**

Baada ya kuutafakari kwa kina utetezi uliowasilishwa na Uongozi wa **EAST AFRICA RADIO**, Kamati ya Maudhui imeridhika pasi na shaka kuwa **EAST AFRICA RADIO** kupitia kipindi chake cha **Supa Breakfast** wamekiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018.

Hivyo basi, Kamati ya Maudhui inatoa adhabu zifuatazo kwa **EAST AFRICA RADIO:**

1. Wanapewa Onyo;

2. Wanatozwa faini ya **Shilingi Milioni Tatu (TZS. 3,000,000.00)** tu itakayolipwa kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA);

Uamuzi huu umetolewa Dar es Salaam leo tarehe **01 Julai, 2020**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia siku ya kutolewa kwa uamuzi huu.

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Joseph Method Mapunda**

**..............................................................**

**Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

**PAMOJA NA WAJUMBE WAFUATAO WA KAMATI YA MAUDHUI:**

**1. Abdul Ramadhani Ngarawa.......................................**

**2. Derek Kaitira Murusuri........................................**

**3. Jacob Gregory Tesha...........................................**